# MUNGU UNIHIFADHI

*Na Sefania Kayala*

***Zab, 16:1-2,5,7-11; (K)1***




**1.Mungu unihifadhi mimi, kwa maana nakukimbilia wewe,**
**nimemwambia Bwana, ndiwe Bwana wangu,**
**Bwana ndiye fungu la posho langu, na la kikombe changu, ki-kombe changu.**

**2.Nitamhimidi Bwana aliyenipa shauri, naam mtima wangu umenifundisha usiku;**
**nimemweka Bwana mbele yangu daima, kwa kuwa yuko kuumeni kwangu,**
**kuumeni kwangu sitaondoshwa.**

**3.Kwa hiyo moyo wangu unafurahi, nao utukufu wangu unashangilia;**
**Naam mwili wangu nao utakaa kwa kutumaini, maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu,**
**wala hutamtoa-, mtakatifu wako aone uharibifu.**

**4.Utanijulisha njia ya uzima, mbele ya uso wako ziko furaha tele,**
**na katika mkono wako wa kuume mna maneno yao mi-le-le-**

**NB: Mashairi yote yafuate tune ya shairi la kwanza pasipo kujali ni refu ama fupi.**

**Kama waimbaji hawataweza kufuata ngoma za kinandampiga kinanda anashauriwa kuzima ngoma ili uimbwe kwa uhuru zaidi (ngoma izimwe wakati wa mashairi tu)**